

Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe

 Fabian Wakholi

 Marleen Visser


 Brigid Simiyu

 Kiswahili

 Level 2

(imageless edition)







Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe
walikuwa marafiki wa karibu sana.
Siku moja walisafiri kwa tekisi.




Walipofika mwisho wa safari yao,
dereva aliwaomba walipe nauli zao.
Ng'ombe alilipa nauli yake.




Mbwa alilipa zaidi kidogo kwa sababu hakuwa na pesa taslimu.




Dereva alipokaribia kumpa Mbwa
chenji yake, Mbuzi alitoroka bila
kulipa chochote.




Dereva alikasirika sana. Aliondoka bila kumrudishia Mbwa chenji yake.



Hiyo ndiyo sababu hadi leo Mbwa hukimbiza magari ili achungulie ndani kuona kama atampata dereva mwenye chenji yake.



Mbuzi hukimbia anaposikia mlio wa gari. Anaogopa atakamatwa kwa kutolipa nauli.



Na Ng'ombe hababaiki gari likiwa linakuja. Ng'ombe huvuka barabara bila wasiwasi kwa sababu anajua alilipa nauli yake yote.



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Mbuzi, Mbwa na Ng'ombe

Written by: Fabian Wakholi

Illustrated by: Marleen Visser

Translated by: Brigid Simiyu

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).